# STANDARD SEVEN MID TERM ONE EXAM 2018
# KISWAHILI

**Jaza pengo kwa jibu ufaalo.**

Mwili wa___1___ una viungo mbalimbali ___2___hufanya ___3___ kwa kushirikiana.Kila kiungo huchangia katika ___4___ jambo fulani, chambilecho wahenga ___5___ ndipo ___6___ uwakapo. Hivi ___7___ binadamu hupaswa kufanya kazi ___8___ ushirikiano na ___9___ .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. insani | B. hayawani | C. watu | D. waja |
| **2.** | A. hufaza | B. hufanya | C. ambavyo | D. ambacho |
| **3.** | A. kasi | B. gange | C. genge | D. kiazi |
| **4.** | A. kuteketeza | B. kuteka | C. kutekeleza | D. kuteka |
| **5.** | A. kinga na kinga | B. papo kwa papo | C. kuko na hupo | D. hapa na hapa |
| **6.** | A. ndoto | B. joto | C. mioto | D. moto |
| **7.** | A. ndipo | B. ndivyo | C. ndimo | D. ndiko |
| **8.** | A. kwa | B. na | C. katika | D. kwenye |
| **9.** | A. utengano | B. utegemeano | C. utangamano | D. utengo |

Kilimo au ___10___ ni sayansi ya kukuza___11___ na___12___ mifugo ___13___ . Ukulima wa ufugaji ___14___ umepwewa ___15___ siku za hivi karibuni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. sanaa | B. zinaa | C. zanaa | D. zaraa |
| **11.** | A. mimea | B. mumea | C. mimeya | D. wanyama |
| **12.** | A. kueka | B. kufuga | C. kufunga | D. kufuka |
| **13.** | A. balibali | B. vingi | C. michache | D. mbalimbali |
| **14.** | A. nsi | B. nswi | C. duara | D. nzige |
| **15.** | A. kipaumbele | B. kipaombele | C. mbele | D. mbee |

***Kutoka nambari 16-30, jibu kulingana na maagizo***

**16.** Tambua salamu ya wakati wote
A. chewa
B. shikamoo
C. cheichei
D. alamsiki

**17.** Sehemu kwenye barabara inapopinda huitwa
A. kona
B. upinde
C. gurufe
D. guruba

**18.** Ufupisho wa mwana wetu ni
A. mwanawe
B. nwanatu
C. mwanetu
D. mwanao

**19.** ***Tambua neno lililopigwa mstari.***
Darasa <u>lile lile</u> ni safi.
A. kiashiria sisitizi
B. kimilikishi
C. kielezi
D. kiwakilishi

**20.** ***Jaza pengo kwa kiunganishi bora***
Ameshindwa kununua baiskeli _______ gari.
A. kefu
B. bali
C. ilhali
D. ingawa

**21.** Kofia nyekundu ambayo inayovaliwa na wanaume waislamu huitwa
A. tarbushi
B. bulibuli
C. taji
D. kidotia

**22.** Tambua <u>pa</u> ya wakati
A. alipolala si pema
B. wamwonapo hucheka
C. akimbiliapo si salama
D. achezeapo ni pabaya

**23.** Ni sentensi gani yenye ki ya ngeli
A. Kitanda chake ni kizuri
B. Kitabu ki kabatini
C. Kijibanda kimeaguka
D. Kipendacho moyo ni dawa

**24.** Kinyume cha ami ni
A. halati
B. bibi
C. shangazi
D. wifi

**25.** Majira ya mvua ndogo huitwa vuli au
A. mchoo
B. rasharasha
C. masika
D. kipupwe

**26.** Kwa kawaida kengele shuleni
A. hupigiliwa
B. hulia
C. hukirizwa
D. hukoroma

**27.** Kauli ya kutendeka ya kitenzi iba ni
A. ibiwa
B. ibisha
C. ibiana
D. ibika

**28.** Kati ya viungo hivi ni kipi si cha upishi?
A. Iliki
B. Jira
C. Mdalasini
D. Biriani

**29.** Mtu anayetoa hotuba huitwa _____ naye anayenadi bidhaa mnadani huitwa _______.
A. hatibu/dalali
B. katibu/dalali
C. mchuuzi/mhutubia
D. katibu/mhariri

**30.** Chagua orodha yenye vielezi pekee
A. soma, lala, omba
B. zuri, baya, choyo
C. ila, ihali, ama
D. ovyo, ghafla, kwa pupa

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 31-40***

Ile ndoto aliyokuwa akiiota miaka mingi Lucy, sasa imepevuka na <u>kujikopoa nje ya akili yake</u>. Hapo alipo, aliiona imemsimamia mbele kwa dhahiri. Ilisimama kwa ukweli usiotatanisha. Kabla ya leo, aliota akining'inia hewani kwenye anga la Uingereza. Nchi anayoijua kwa picha zinazotembea kwa rangi tofauti ili kumwonjesha yeye utamu wa London. London na barabara zake pana zinazojaa magari na <u>watu pomoni</u> wanaokwenda na kurudi kike na kiume, vijana na wazee - wote waliovaa kifahari na kitajiri. Maduka mengi yaliyopachanapachana ambayo hujaa bidhaa za kila aina. Mikahawa ya vyakula na mahoteli na majumba marefu

marefu wanamoishi watu wake na viwanja vya nafasi yenye kuitwa *squares* na mabustani makubwa yanayowanda kaskazini hadi kusini: nafasi za kazi, utajiri, raha, anasa, muziki na hasa madisko na sinema.... haishi Uingereza kuipaka rangi zinazomemeteka.

Mambo si hayo! Usije kabisa ukamwambia Lucy kuwa hiyo yake ni ndoto tu. Atagombana na wewe na kukwambia wazi kwamba wewe umegeuka sungura aliyekosa zabibu. Yeye si kwamba ameoteshwa lakini anajua kwamba kiwiliwili chake kila siku huruka angani kuenda kutua na kuikagua Uingereza-hasa London. Nani basi atamwambia vingine na yeye ameiona kwa macho yake ingawa ndotoni? Yeye anaamini siku moja itakuwa siku, maana hizi zote ni mafigu tu, haziishi kuporomoka!

Basi siku zote hizo kiu ya kuenda kuishi London ilikuja kumkaa ikamchagiza kama vile kiu ya mtu alikuwa akisafiri jangwani kwa miaka bila ya kuyagundua maji. Lini atayaona maji? Alijiuliza. Lini ataiona London? Lini atafika London? Alijua kwamba jibu la suala hili ni gumu, lakini hakukata tamaa. Aliamini kwa jinsi yeye mwenyewe alivyo, akitaka kitu lazima akipate. Alikuwa na hakika kwamba miujiza itazuka tu kwa njia yoyote ingawa hajui ipi.

**31.** Lucy aliota ndoto ya kwenda wapi haswa?

A. Uzunguni
B. Uingereza
C. ughaibuni
C. Uropa

**32.** Maneno haya kujikopoa nje ya akili yake yana maana

A. ndoto haikutimia
B. ilikuwa ni jinamizi
C. kukosa kufikirika
D. ndoto ilidhirika vyema

**33.** Mwandishi aliota ndoto hii lini?

A. Leo
B. Jana
C. Juzi
D. Mtondogoo

**34.** Kulingana na aya ya pili barabra za London

A. zina waja wachache
B. si baraste
C. zina watu sisisi
D. magari ni machache

**35.** London kunapatikana haya yote sipokuwa

A. kazi
B. anasa
C. utajiri
D. fujo na vurugu

**36.** Mwandishi amefika London kwa kupitia njia ya

A. kusafiri kwa ndege
B. baraste
C. maoni
D. ndotoni

**37.** Kulingana na kisa hiki kiu ya Lucy ya kwenda London inaliganishwa na

A. tamaa ya fisi
B. mkamia maji
C. msafiri jangwani kwa mwaka bila kuwahi maji
D. msafiri aliyepata maji jangwani

**38.** Mwandishi anajiuliza maswali mangapi kuhusu kiu yake ya kwenda London?

A. Mengi
B. Mawili

C. Machache

D. Kadha wa kadha

**39.** Tamati ya habari hii ni kwamba Lucy

A. alipoteza matumaini

B. alitamani lakini alikufa moyo

C. alitupilia mbali ndoto yake

D. ana matumaini na imani kuwa atatia guu lake kule

**40.** Habari hii inatupatia funzo kuwa

A. Tusiote ndoto za mchana

B. Tuwe na ndoto zenye maono

C. Ndoto na maono ni muhimu

D. Ndoto hihutaji uvumilivu na subira ili kufaulu

***Soma habari hii na kisha ujibu maswali 41-50.***

Miti hutumika kutupatia moto ingawa kunazo njia nyingine tumbi nzima za kujipatia moto. Utaona kwamba kuni kutoka mitini hutumika kwa wingi. Hususan walalahoi kama mimi hutumia kuni na makaa kwa mahitaji ya moto. Tunatumia moto kwa njia tele kama vile kupikia, kupasha maji moto kuota nikitaja tu chache.

Mazingira yetu huboreshwa na miti. Ni jambo bayana kuwa, miti hutoa hewa tunayoitumia kupumulia na wakati huo 'hufyonza' hewa chafu. Jambo hili huchangia si haba katika uhifadhi wa hewa safi. Aidha miti inasaidia katika upataji wa mvua ya kutosha. Wanasayansi huamba kuwa jua lichomapo baadhi ya maji hupaa kutoka mitini katika hali ya mvuke. Baadaye mvuke huo huganda na kudondoka ukiwa ni mvua. Ni nani asiyejua faida ya mvua?

Miti huzuia mmomonyoko wa udongo. Utaona ya kwamba, miti hupunguza kasi ya matone ya mvua na ya upepo. Kutokana na upunguzaji huo wa kasi, basi maji au upepo haviwezi kuunyonyoa udongo wetu. Yafaa ikumbukwe kwamna taifa letu hutegemea kilimo na iwapo udongo utaharibiwa basi hatutakuwa na tumaini la kupata chakula. Tutakuwa tukitegemea misaada au mikopo na kama walivyonena wahenga, nguo ya kuazima haifichi mwili.

Miti pia huchangia kuboresha udongo wetu. Majani ya miti yanapopukutika huoza na kuongeza rotuba udongoni. Jambo hili huchangia kupata mavuno mema.

Si hayo tu, miti ni maskani ya wanyama chungu nzima. Wanyama hao huvutia watalii wanaotuletea pesa za kigeni. Kutokana na pesa hizo tunapiga hatua mbele kimaendeleo na hata kupiga teke ufukura. Pesa hizo hutumiwa kutengenezea barabra, miundo msingi na huduma nyingine za umuhimu.

Wahenga waliamba, aisifuye mvua imemnyea. Ninaisifu miti kwa kuwa nimeona faida zake. Hata hivyo wahenga wale walisema kwamba hakuna kizuri kisicho na ila. Miti ina mabaya lakini machache.

Miti mingine huwa na sumu na tunapokula majani na matunda basi tunaathirika. Aidha, miti ni makao ya wanyama ambao wengine hutishia aushi ya binadamu.

Aghalabu mnamo misimu ya masika miti huanguka na kusababisha hasara. Kwa mfano, miti huangukia watu, nyumba, nyaya za stima na simu na hata magari. Fauka ya hayo, mara kwa mara mizizi ya miti huharibu nyumba zetu. Hususan miti inapomea karibu na nyumba inaweza kuathiri udhabiti wa nyumba.

Licha ya hasara za miti, ni bayaba kuwa, faida zake hazina kifani. Ni wajibu wetu tuongeze na tuihifadhi miti yetu. Kamwe tusiongozwe na tamaa na kuwa vipofu wa kuharibu miti. Iwapo tunafanya hayo, tutakuwa tumejipalia makaa na tusitarajie pole kwani mwiba wa kujidunga hauambiwi pole.

**41.** Mwandishi anawataja nani kuwa ndio wanaotumia kuni na makaa zaidi

A. walalaheri

B. walalahoi

C. matajiri

D. kila binadamu

**42.** Katika aya ya kwanza tumetajiwa njia ngapi ambazo moto hutumika

A. tano

B. chache tu

C. tatu

D. nne

**43.** Mazingira yetu huboreshwa na miti

A. inapofyonza hewa chafu

B. inapotoa hewa chafu

C. tunapoikata miti iliyosongamana

D. inapofyonza hewa safi

**44.** Wanasayansi wanatudokezea kuwa _____

A. miti hutumia maji mengi

B. maji huenda hewani kama mvuke kutoka kwenye miti

C. mvua hunyesha kusiko na miti

D. mvuke huganda kwenye miti

**45.** Mwandishi anaelezea nini anaposema <u>nguo ya kuazima isiyositiri uchi</u>

A. misaada na mikopo

B. mikopo kutoka kwa watalii

C. misaada kutoka nchi za nje

D. pesa za kigeni

**46.** Madhara yanayoweza kusababishwa na miti ni haya isipokuwa

A. miti yenye sumu

B. makazi ya wanyama hatari

C. Utalii na pesa za kigeni

D. kuanguka kwa miti na kuleta hasara

**47.** Watalii hutuletea faida gani nchini

A. pesa za mikopo

B. pesa za kigeni

C. usaidizi wa kimaendeleo

D. bidhaa za kigeni

**48.** Faida zake hazina kifani, maneno haya yana maana ya

A. faida zisizo na mfanowe

B. faida anuwai

C. faida kichele

D. faida kiasi cha haja

**49.** Kati ya mambo haya ipi si sehemu ya mazingira muhimu?

A. Hewa

B. Maji

C. Miti

D. Gesi zenye sumu

**50.** Habari hii ni kuhusu

A. Mazingira yetu

B. Umuhimu wa mazingira

C. Kutunza miti yetu

D. Miti na umuhimu wake